**Mwongozo Mfupi wa Malalamiko**

## Yale Tume hutekeleza

Tume ya Haki za Binadamu ya Australia ni shirika linalojitegemea, la kitaifa, ambalo huchunguza na kufupisha malalamiko ya ubaguzi na ukekuaji wa haki za binadamu na Jumuiya ya madola katika hali zingine. Tume hutendakazi kwa njia isiyo ya upendeleo na haifanyikazi kwa ajili ya pande zote za malalamiko. Mwongozo huu unaweza kukusaidia ikiwa unataka kutoa malalamiko.

Tume huendesha sheria tano tofauti. Sheria hizi ni:

- *Sheria ya 1975 ya Ubaguzi wa Kimbari*
- *Sheria ya 1984 ya Ubaguzi wa Kijinsia*
- *Sheria ya 1986 ya Tume ya Haki za Binadamu ya Australia*
- *Sheria ya 1992 ya Ubaguzi wa Ulemavu*
- *Sheria ya 2004 ya Ubaguzi wa Umri*

## Mbari

*Sheria ya 1975 ya Ubaguzi wa Kimbari* huifanya kinyume cha sheria kwa watu kutendewa vibaya kwa sababu ya umbari wao, rangi, ukoo au taifa au asili ya kijamii katika maeneo mengine ya maisha ya umma, kama vile ajira na katika upeanaji wa bidhaa na huduma. Sheria pia inakataza chuki ya kimbari. Hii hutendeka wakati mtu anapofanya, anaposema au kuchapisha jambo fulani adharani hambalo linaweza kukukasirisha, kukuaibisha au kukuogofya kwa sababu ya umbari wako, rangi au taifa au asili ya kijamii.

## Jinsia

*Sheria ya 1984 ya Ubaguzi wa Kijinsia* huifanya kinyume cha sheria kwa watu kutendewa vibaya kwa sababu ya jinsia yao, hali ya ndoa au ujauzito katika maeneo mengine ya maisha ya umma, kama vile ajira na katika upeanaji wa bidhaa na huduma. Pia ni kinyume cha sheria kumfuta mtu kazi kwa sababu ya uwajibikaji wa familia yao. Sheria pia inakataza uyanyasaji wa kingono katika maisha ya umma. Unyanyasaji wa kingono ni tabia isiyokubaliwa ya tabia ya kingono ambayo mtu timamu anaweza kupata kuwa ya kuchukiza, ya kufedhehesha au ya kuogofya.

## Ulemavu

*Sheria ya 1992 ya Ubaguzi wa Ulemavu* huifanya kinyume cha sheria kwa mtu aliye na ulemavu kutendewa vibaya kuliko mtu mwingine ambaye hana ulemavu huo katika maeneo mengi ya maisha ya umma, kama vile ajira, elimu, ufikiaji wa rasilimali na katika upeanaji wa bidhaa na huduma. 'Ulemavu' hufafanuliwa kwa upana sana na unajumuisha aina zote za ulemavu wa kimwili na kiakili na kuwepo kwa ogani zinazobeba maradhi mwilini.

Sheria pia inajumlisha ulemavu ambao unao sasa, umekuwa nao zamani, unaoweza kuwa nao katika maisha ya usoni au unaoaminika kuwa nao. Pia inajumlisha vifaa, wasaidizi au wanyama waliofunzwa ambao unaweza kuwa nao kwa sababu ya ulemavu wako.

## Umri

*Sheria ya 2004 ya ubaguzi wa Umri* huifanya kinyume cha sheria kuwatendea watu vibaya kwa sababu ya umri wao katika maeneo mengine ya maisha ya umma, kama

vile ajira, katika upeanaji wa bidhaa, huduma au vifaa, makazi, elimu na katika kusimamia sheria na mipango ya Jumuiya ya madola.

Maeneo mengine ya maisha ya umma huruhusu Sheria hii kama vile faida ya kustaafu, uhamiaji, ushuru, mshahara wa vijana na sheria za jimbo. Pia si kinyume cha sheria kupeana faida kwa rika maalum ambapo imekusudiwa kufikia hitaji ambalo huzuka kutoka kwa rika hilo.

**Haki za Binadamu na Ajira**
*Sheria ya 1986 ya Tume ya Haki za Binadamu ya Australia* hujumlisha maeneo mawili muhimu ya malalamiko. Eneo la kwanza hushughulika na ukeukaji unaodaiwa wa haki za binadamu au kwa niaba ya Jumuiya ya madola ya Australia. Haki za binadamu hufafanuliwa kama zile ziliyomo katika mikataba ya kimataifa na maazimio ambayo yamepangwa au kusemwa chini ya Sheria hii, kama vile *Mapatano ya Kimataifa ya Haki za Kiraia na Kisiasa* na *Mkutano juu ya Haki za Watoto.*

Eneo la pili la malalamiko ni kutendewa vibaya katika ajira na kikazi kwa misingi ya kidini, maoni ya kisiasa, asili ya kijamii, umri, rekodi ya uhalifu, upendeleo wa ngono au shughuli ya chama cha wafanyakazi.

**Kuondolewa, kuruhusiwa na ulinzi**
Sheria zote zilizotajwa hapo juu hupeana ruhusa kadhaa na kuondolewa kwa kuwa sio kutendewa kote kubaya ni kinyume cha sheria. Pia kuna ulinzi kadhaa unaopatikana kwa wenye kujibu.

**Kutoa malalamiko**
Tume hupeana huduma ya bure ya malalamiko. Unaweza kuwasiliana na Tume kwa ajili ya ushauri na usaidizi kwa shida ambayo unahisi imesababishwa na ubaguzi au ukeukaji wa haki zako za binadamu.

Hakuna haja yako ya kuwa na mwakilishi wa kisheria. Uamuzi wa kumhusisha au kutomhusisha wakili ni wa upande unaohusika. Walakini, unapaswa kugundua kuwa Tume haipeani usaidizi wo wote wa kifedha kwa uwakilishi wa kisheria.

Malalamiko mengi huanza na kupiga simu kwa Tume. Afisa wa habari ya malalamiko atakusaidia kuamua kama malalamiko yako yatashughulikiwa na Tume au hapana. Ikiwa ni hivyo, utashauriwa hatua inayofuata utakayoichukua. Tume ina TTY na huduma ya kukalimani lugha inayopatikana kwa maswali ya simu.

- Namba ya Laini ya Maelezo ya Malalamiko ni 1300 656 419.

- Namba ya Huduma ya maelezo ya Utafsiri ni 13 14 50.

**Kutoa malalamiko kwa Tume**
Isipokuwa kwa hali zingine maalum, malalamiko yote kwa Tume yanapaswa kuandikwa. Hii inaweza kuwa kwa aina yo yote ya kuandikwa (ikijumuisha barua pepe) na kwa lugha yo yote. Tume ina fomu za malalamiko zinazopatikana. Ijapokuwa si lazima utumie fomu ya malalamiko, ni muhimu sana kwa sababu inaorodhesha habari zote unazohitajika kutuambia unapokua ukitoa malalamiko. Unapaswa kutuma malalamiko yako kwa:

The Director – Complaint Handling
Australian Human Rights Commission
GPO Box 5218
Sydney NSW 2001

**Vile malalamiko yako yatakavyoshughulikiwa**
Njia ya malalamiko ni rahisi, lakini kwa kawaida malalamiko mengi hushughulikiwa kwa njia zifwatazo.

Malalamiko yote yanayopokewa na Tume huchunguzwa na Mkurugenzi, Ushughulikiaji Malalamiko.

Wafanyakazi wa Tume wanaweza kuwasiliana na wewe kwa habari zaidi. Baada ya hiyo (kama itaamuliwa kuwa malalamiko yako yanahitaji kuchunguzwa), Tume itamwandia mwenye kujibu (mtu au shirika unalolalamika kuhusu) na itawapa nakala ya malalamiko na watafute maoni yao juu ya malalamiko kwa kuuliza maswali mengine. Mwenye kujibu kwa kawaida atakuwa na siku ishirini na moja (21) ambazo atapaswa kujibu maswali ya Tume. Kwa kawaida utapewa nakala ya majibu.

Baada ya uchunguzi na habari zinazolingana kupatikana, Rais ataamua kama:

- kuondoa (kufunga) malalamiko, au
- ajaribu kutatua malalamiko kupitia upatanisho.

Upatanisho hufanyika wakati Tume na mwenye kulalamika na mwenye kujibu wakifanyakazi pamoja ili kujaribu kupata suluhisho ambalo pande zote zinaweza kukubaliana. Njia ya upatanisho hupeana fursa kwa pande zote kupeana hadithi ya upande wao bila ya kwenda kortini, na kutatua malalamiko kwa njia ya kawaida na kwa masharti ambayo pande zote zinaweza kukubaliana.

Upatanisho unaweza kufanywa na mtu mwenyewe, kwa kuandika, au kwa simu.

**Misingi ya kuondoa malalamiko**
Ikiwa malalamiko hayatatatuliwa kupitia upatanisho, Rais ataondoa malalamiko.

Rais pia anaweza kuondoa malalamiko kwa sababu zingine, ikijumuisha kuwa ameridhika kwamba:

- kitendo kinacholalamikiwa si kinyume cha sheria;
- malalamiko yalitolewa zaidi ya miezi kumi na mbili (12) baada ya ubaguzi unaodaiwa kutendeka;
- malalamiko yanakosa msingi;
- kuna urekebisho mzuri ambao unaweza kutumiwa, au;
- jambo hilo ni swala muhimu kwa umma ambalo linapaswa kushughulikiwa na Mahakama ya Muungano wa Australia.

Mara malalamiko chini ya *Sheria ya 1975 ya Ubaguzi wa Kimbari, Sheria ya 1984 ya Ubaguzi wa Ulemavu* au *Sheria ya 2004 ya Ubaguzi wa Umri* inapoondolewa, Rais atapeana ‘Ilani ya Kuondolewa’. Hii itakuruhusu kupeana maombi kwa Mahakama ya Muungano wa Australia kwa ajili ya kusikilizwa na kuondolewa. Tume haiwezi

kukusaidia kuendesha kesi yako mahakamani. Unapaswa kugundua kuwa ikiwa hautafaulu, itakubidi ulipie gharama ya upande ule mwingine.

Ikiwa jambo hilo liko chini ya *Sheria ya 1986 ya Tume ya Haki za Binadamu ya Australia*, kuhusu ukeukaji uliodaiwa wa haki za binadamu au ubaguzi katika ajira au kikazi, Rais anaweza kukataa kuendelea na maswali yake kwa misingi sawa na yale yaliyoorodheshwa hapo juu. Walakini, hakuna hatua ya mahakama inayopatikana chini ya Sheria hii. Kama Rais ataamua kuwa kumekuwa na ukeukwaji wa haki za binadamu au ubaguzi umetendeka, ni lazima aripoti kwa Mkuu wa Sheria na anaweza kupendekeza hali irekebishwe. Mkuu wa Sheria ni lazima awasilishe ripoti hii kwa Bunge.

**Jinsi ya kuwasiliana na Tume**

- Laini ya Habari ya Malalamiko 02 9284 9600 au 1300 656 419 (gharama ya simu ya mahali ulipo).
- Namba ya TTY ni 1800 620 241.
- Huduma ya Utafsiri na Habari 13 14 50 (kwa ajili ya ukalimani wa lugha)
- Barua pepe complaints.info@humanrights.gov.au
- Tovuti www.humanrights.gov.au

Tafadhali elekeza mawasiliano yote kwa:
Director – Complaints Handling
Australian Human Rights Commission
Level 8, 133 Castlereagh Street
Sydney NSW 2000

au

GPO Box 5218
Sydney NSW 2001